# CLASS 5 MID TERM 2 2020

# KISWAHILI

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.**

Usiku __1__ mama yetu __2__ chakula __3__ sana. Tulikula hadi tukashiba ndi! Baada ya __4__ meza, vyombo vilipelekwa jikoni ambako __5__ wetu alianza kuviosha. Baba alianza __6__ taarifa za habari kwenye runinga yetu mpya. Mimi nilitulia kwenye __7__ kwa kuwa nilikuwa nimemaliza kufanya kazi __8__ ziada. Ghafla bin vuu, mvua __9__ kunyesha. Mabati __10__ kelele hadi baba akaizima runinga. Mara maji ya mvua yalianza kuingia __11__ ya nyumba. Maji __12__ yalikuwa baridi kama __13__. Baba __14__ jembe na kuenda huko nje, alilima kandokando ya nyumba __15__ maji yasiingie. Baadaye aliufunga mlango. Kila mmoja alienda kulala fofofo.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. huyo | B. huo | C. hiyo | D. hizo |
| 2. | A. aliwapikia | B. alitupikia | C. alimpikia | D. alinipikia |
| 3. | A. kitamu | B. tamu | C. nzuri | D. mzuri |
| 4. | A. kupangusha | B. kupanguza | C. kupangunza | D. kupangusa |
| 5. | A. dereva | B. daktari | C. yaya | D. topasi |
| 6. | A. kuona | B. kutazama | C. kuangalia | D. kusikia |
| 7. | A. meza | B. kinu | C. rafu | D. kochi |
| 8. | A. ya | B. wa | C. cha | D. vya |
| 9. | A. ilianza | B. ulianza | C. kulianza | D. mlianza |
| 10. | A. ulipiga | B. lilipiga | C. yalipiga | D. zilipiga |
| 11. | A. juu | B. ndani | C. kando | D. chini |
| 12. | A. hayo | B. hiyo | C. hizo | D. huo |
| 13. | A. maziwa | B. usiku | C. barafu | D. maji |
| 14. | A. alichukuwa | B. atachukua | C. atachukuwa | D. alichukua |
| 15. | A. ila | B. bali | C. lakini | D. ili |

**Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.**

16. Chagua sentensi ambayo ni sahihi.
    A. Mtoto yoyote asichezee uwanjani.
    B. Kitabu kingine kimenunuliwa.
    C. Darasa lenye limeoshwa ni letu.
    D. Mawazo nyingi yanamsumbua.
17. Nomino gani ambayo haipatikani katika ngeli ya **U - ZI** kati ya hizi?
    A. Nyumba.
    B. Nyufa.
    C. Nyuso.
    D. Nywele.
18. Jina lingine la **surupwenye** ni
    A. kizibao
    B. shimizi
    C. bwelasuti
    D. joho
19. Chagua wingi wa:
    **Daktari huyu ni wangu.**
    A. Madaktari haya ni yetu.
    B. Madaktari hawa ni wetu.
    C. Madaktari hao ni wangu.
    D. Daktari hawa ni wetu.


20. Orodha gani iliyo na vivumishi vya sifa pekee?
A. kimoja, vichache, kumi.
B. hizo, huyo, lile.
C. -ote, -o-ote, -enyewe.
D. mzuri, safi, wabaya.

21. Mmea ambao zao lake ni ndizi huitwaje?
A. Mbuni
B. Mpunga
C. Mpareto
D. Mgomba

22. Chagua sentensi iliyo katika hali ya mazoea.
A. Punda wetu hupumzika kila Jumamosi.
B. Nitapanda miti pale shambani.
C. Walienda Mombasa kumtembelea mjomba.
D. Simu ile mpya imewekwa.

23. Tambua ukanusho wa:
**Nimekula ugali na kunywa chai.**
A. Sijakula ugali na sikunywa chai.
B. Nimekula ugali lakini sikukunywa chai.
C. Sijala ugali na sijanywa chai.
D. Sijala ugali wala sijanywa chai.

24. Umbo hili huitwaje?



A. Mche.
B. Pia.
C. Mistari sambamba.
D. Mraba.

25. Chagua sentensi iliyotumia **'ji'** kuonyesha ukubwa.
A. Jibwa la baba limelala.
B. Uimbaji wako ni mzuri.
C. Mtoto amejiangusha chini.
D. Wachezaji wale wamecheza vizuri.

26. Alama gani ambayo ni **'hisi'** kati ya hizi?
A. **?** B. **!**
C. **,** D. **.**

27. Sentensi gani ambayo maneno yamepangwa vizuri?
A. Mchuuzi ana ujuzi wa kuuza mchuzi.
B. Kuuza mchuzi wa ujuzi ana mchuuzi.
C. Mchuzi ana ujuzi wa kuuza mchuuzi.
D. Ujuzi wa kuuza mchuzi ana mchuuzi.

28. **'Kabla ya, kati ya, baada ya'** ni mifano ya:
A. viunganishi
B. vihusishi
C. vuonyeshi
D. viwakilishi

29. Sentensi ipi iliyotumia kiulizi kwa usahihi?
A. Mnyama myupi atakayechinjwa?
B. Vijiko vigani vilivyooshwa jana?
C. Kalamu zake ni zingapi?
D. Mguu upi ulioumia?

30. Jibu lipi lililolinganisha kiumbe na makao yake inavyofaa?
A. Kuku - mzinga
B. Samaki - zizi
C. Konokono - kombe
D. Ndege - kizimba

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kutoka 31 hadi 40.</u>***

Usafi ni hali ya kutokuwa mchafu au kutokuwa na uchafu karibu na wewe. Hii inamaanisha kuwa usafi unahusu mwili wako na mazingira yako. Je, usafi una faida gani katika maisha yetu? Kwa nini ni muhimu kuwa safi au kuishi mahali ambapo ni safi? Jambo la kwanza ni kuwa usafi hutuepushia magonjwa. Kuna magonjwa ambayo husababishwa na uchafu. Magonjwa hayo ni kama vile kipindupindu, kuendesha, kichocho na malaria. Pengine unashangaa ni jinsi gani uchafu husababisha malaria na kichocho. Konokono na mbu ambao huambukiza magonjwa haya hupenda sana kuishi katika maji machafu.

Sababu nyingine ni kuwa usafi hutuepusha na wanyama na wadudu hatari. Wanyama kama vile nyoka na panya hupenda mahali penye uchafu. Nyoka ambao wana sumu wakimwuma mtu, sumu hiyo inaweza ikamsababishia kifo. Wadudu kama vile nzi, mende,

chawa na kunguni nao wana madhara mengi kwa afya ya binadamu. Panya nao ni waharibifu sana kwa vitu vinavyopatikana nyumbani. Panya hutoboa nguo, viti na magunia yenye vyakula. Panya pia huharibu vyakula mbalimbali katika nyumba.

Harufu mbaya iletwayo na uchafu humfanya mtu ashindwe kupumua. Vilevile, ni vigumu sana kufanya kazi katika mazingira machafu. Kuna wakati ambapo watu huangushwa na uchafu na hata kuumia. Hili linamaanisha kuwa usafi hutusaidia kufanya kazi bila matatizo. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa tunakuwa safi na mazingira yetu pia ni safi.

---

**31.** Kulingana na ufahamu, usafi ni nini?
- A. Ni hali ya kuwa mchafu au kutokuwa na uchafu.
- B. Ni hali ya kutokuwa mchafu.
- C. Ni hali ya kutokuwa na uchafu.
- D. Ni hali ya kutokuwa mchafu au kutokuwa na uchafu tupokaa.

**32.** Usafi unahusu nini?
- A. Mwili na mazingira.
- B. Meno na uso.
- C. Nyumba na madarasa.
- D. Mazingira na soko.

**33.** Katika aya ya kwanza, usafi hutuepushia nini?
- A. Wadudu hatari.
- B. Magonjwa.
- C. Wanyama hatari.
- D. Wadudu na wanyama hatari.

**34.** Ugonjwa gani kati ya haya ambao husababishwa na kiumbe anayependa kuishi katika maji machafu?
- A. Kichocho
- B. Kifafa
- C. UKIMWI
- D. Kifaduro

**35.** Ni nini ambacho huharibu vitu vinavyopatikana nyumbani kulingana na ufahamu?
- A. Nzi  B. Mende
- C. Panya  D. Nyoka

**36.** Usafi huweza kutuepusha na mnyama gani?
- A. Nyoka  B. Chawa
- C. Kunguni  D. Nzi

**37.** Harufu mbaya iletwayo na uchafu humfanya mtu ashindwe kufanya nini?
- A. Kutembea.  B. Kuona.
- C. Kuongea.  D. Kupumua.

**38.** Uchafu gani ambao unaweza ukamwangusha mtu kwa urahisi kati ya huu?
- A. Vumbi  B. Moshi
- C. Mchanga  D. Ganda la ndizi

**39.** Kazi ya kuhakikisha kuwa tunadumisha usafi ni ya nani?
- A. Walimu  B. Wanafunzi
- C. Kila mtu  D. Wazazi

**40.** Ufahamu huu unahusu nini?
- A. Afya  B. Usafi
- C. Wadudu  D. Magonjwa

---

***Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

SHULE YA JUHUDI,
S.L.P 836,
HURUMA.
3/3/2020.

Kwa mwanangu Maria,

Hujambo mwanangu? U hali gani? Unaendeleaje huko shuleni? Sisi huku nyumbani tu wazima. Baba yako na ndugu zako nao wanaendelea vyema. Bibi yako aliyekuwa akiugua ugonjwa wa malaria amepona baada ya kupelekwa zahanatini. Wote wamesema kuwa nikusalimie.

Lengo au sababu ya kukuandikia barua hii ni kukushauri kuhusu faida za elimu. **Nilipigiwa** simu na mwalimu wako wa darasa hapo jana, akaniambia kuwa huko shuleni **unachezacheza** tu na kulala ovyoovyo. Jambo hilo lilinihuzunisha sana. Mwalimu aliniambia **kuwa** hata ukishauriwa kuwa tabia hiyo ni mbaya husikii. Je, hujui kuwa **asiyesikia la mkuu huvunjika guu**?

Faida ya kwanza ya elimu ni kuwa huondoa ujinga. Mtu anaposoma, tabia mbalimbali za kipumbavu huondoka. Kuchezacheza shuleni kunaonyesha kuwa hujui faida hiyo ya masomo. Shuleni, tabia zako zinafaa kuwa tofauti sana. Mtu aliyesoma anafaa kuwa **mwenye bidii kama mchwa**. Usiwe mzembe hata kidogo. Mimi na baba yako hatukupata nafasi ya kusoma, mbona wewe unaichezea nafasi hiyo? Mwanangu, usiyachezee masomo hata kidogo.

Kwa kuwa giza limeanza kuingia, nitakomea hapo. Kumbuka hili si darasa la nne ulimokuwa mwaka jana. Miaka inasonga haraka sana. Tutaonana shule zikifungwa, jikaze mno upate matokeo bora wakati wa mtihani wa mwisho wa muhula. Kwaheri ya kuonana.

Ndimi mzazi wako mpendwa,
Salama Zuri.

---

**41.** Mwandishi wa barua hii anaishi katika mji gani?
A. Nairobi
B. Nyumbani
C. Huruma
D. Shuleni

**42.** Inawezekana kuwa barua hii iliandikwa muhula gani?
A. 3
B. 2
C. 1
D. 2020

**43.** Ni nani aliyekuwa akiugua ugonjwa wa malaria kulingana na ufahamu?
A. Maria
B. Mke wa Maria
C. Mama wa Maria
D. Nyanya wa Maria

**44.** Barua hii imeandikwa ili kutoa ushauri kuhusu nini?
A. Faida za kusoma.
B. Umuhimu wa amani.
C. Umuhimu wa kilimo.
D. Jinsi ya kupita mtihani.

**45.** Ni nani aliyepiga simu kulingana na ufahamu?
A. Maria
B. Mzazi wa Maria.
C. Mwalimu wa Maria.
D. Rafiki wa Maria.

**46.** Methali, **'asiyesikia la mkuu huvunjika guu'** inashauri kuwa:
A. tusome kwa bidii
B. tufuate tunayoambiwa na wakubwa wetu
C. tuwe na marafiki wazuri
D. tuende shuleni mapema.

**47.** Maneno **'mwenye bidii kama mchwa'** ni mfano wa
A. nahau
B. kitendawili
C. fumbo
D. tashbihi

**48.** Mwandishi wa barua hii ni nani?
A. Maria.
B. Baba wa Maria.
C. Mama wa Maria.
D. Mwalimu wa Maria.

**49.** Inawezekana kuwa barua hii iliandikwa wakati gani?
A. Asubuhi
B. Jioni
C. Mchana
D. Usiku

**50.** Aliyeandikiwa barua hii yuko katika darasa lipi?
A. 5
B. 4
C. 3
D. 6